

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TATU**

**20 MEI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU – TAREHE 20 MEI, 2026

I. **DUA:**

II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**386. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (CHAMAZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mzambarauni - Mkoroshini – Saku Store – Saku Mwisho hadi Daraja la Kirungule iliyopo kwenye Mradi wa DMDP.

**387. MHESHIMIWA AMINA MUSSA MKUMBA (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaikarabati Barabara ya Kipoka – Mahimbwa kwa kiwango cha changarawe ili kufungua Kata za Delta.

**388. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Soko la kisasa Kayanga ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**389. MHESHIMIWA DKT. CATHERINE CANUTE JOACHIM (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, utekelezaji wa Mfumo wa Serikali Mtandao umefanikiwa kwa kiwango gani katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa Wananchi.

**WIZARA YA MADINI:**

**390. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Wananchi wa eneo la Mgodi wa Makaa ya Mawe Ketewaka watalipwa fidia ili waachie eneo hilo na kufanya shughuli zao maeneo mengine.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**391. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege Mwada Mkoani Manyara.

**WIZARA YA MAJI:**

**392. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIM HALAMGA (HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itajenga Mradi wa Maji Basout.

**393. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mkandarasi wa Mradi wa kupeleka maji Malampaka na Malya atalipwa fedha zake ili kukamilisha Mradi huu.

**394. MHESHIMIWA SALMA RASHID KIKWETE (MCHINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali italetta fedha za kumaliza Mradi wa Maji Awamu ya Pili katika Jimbo la Mchinga.

**WIZARA YA KILIMO:**

**395. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itachukua Mashamba ya Chai ya Mohamed *Enterprises* zaidi ya Hekta 2000 ambayo yamekuwa mapori na kuwagawia Wananchi.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**396. MHESHIMIWA MARIRTA GIDO KIVUNGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaendeleza maeneo ya Wafugaji kwa kutenga maeneo ya malisho na kujenga Mabwawa ya Mifugo - Longido.

**WIZARA YA UJENZI:**

**397. MHESHIMIWA DKT. YAHAYA ESMAIL NAWANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Taa za Barabarani katika Mji wa Kitangari.

**398. MHESHIMIWA KIZA HUSSEIN MAYEYE (KIGOMA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Bubango Chankele - Kagunga kwa kiwango cha lami.

**399. MHESHIMIWA ZUBERI YAHYA MFAUME  
(MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara kutoka Msalabani hadi Tawa utaanza.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA UJENZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA  
20 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**